


Wanafunzi kutoka JSEC wanajitayarisha kuongea katika mkutano wa Baraza la Shule mwezi Mei tarehe 18.

# MIUNGANISHO

MEI 27, 2022

## KONA YA AFISA MKUU MSIMAMIZI



**DKT. JAVIER MONTAÑEZ**
Afisa Mkuu Msimamizi

Karibu kwenye toleo la mwisho la Shule ya Umma ya Wilaya ya Providence (PPSD) kijarida cha mara mbili kwa wiki. Ikiwa wewe au mtu unayemjua atakosa mojawapo ya majarida yetu, unaweza kupata matoleo ya awali kwenye tovuti ya PPSD katika lugha nyingi.

Wiki hii sote tulikuwa na hofu kuhusu upigaji risasi wa kutisha shuleni huko Uvalde, Texas. Mawazo yetu yako kwa waathirika na wapendwa wao wakati huu mgumu mno wa majonzi na uchungu.

Msiba huu huko Texas kwa uhakika umeleta maswali kuhusu usalama shuleni mwetu nchini kote. Washirika wengi wa jamii ya PPSD wamewasiliana nami wakiniuliza kuhusu miundo na mikakati yetu hapa Providence. Hapa chini ni baadhi ya maelezo hayo, ili uweze kupata ufahamu kuhusu jinsi tunavyofanya kazi kuweka wanafunzi na wafanyakazi wetu salama.

Mpango wetu wa kushughulika na hali ya dharura usimamizi umejengwa kwa ushirikiano wa Idara ya Polisi ya Providence, Idara ya Wazima Moto ya Providence na Wakala wa Usimamizi wa Dharura wa Providence. Mpango huu unatoa mfumo kulinda wanafunzi na wafanyakazi na unaorodhesha majukumu ya wafanyakazi wakati wa hali za dharura 36 tofauti. Tunahitajika kutathmini na kusasisha mpango huu kila baada ya miaka mitatu, na tutafanya hivyo majira haya ya joto.

Walimu Wakuu wa Shule za Umma za Providence wanahitajika kuanzisha "eneo la chuo lililofungwa" katika majengo yao kwa kuweka mlango mmoja tu kwa kuingilia na kutokea ikiwa itawezekana. Wageni wote ni sharti watie sahihi wakiingia na watie sahihi wakitoka ofisi ya shule, na mtu yeyote asiye idhinishwa shuleni anahitaji kushughulikiwa mara moja na kupigia simu 9-1-1 ikiwa itahitajika.

Wilaya inafanya majaribio ya mikakati kadhaa ya mifano ya dharura na usalama kila mwaka, ikijumuisha kuondoa watu na ufungaji maeneo. Tunatumia mfumo ambao unafanana sana na itifaki ya ALICE kama mwitikio dhidi ya mvamizi yeyote mwenye silaha. Mfumo huu umeundwa kutoa utayari kamili ikiwa kutakuwa na mvamizi katika moja ya shule zetu.

Kama utakavyo ona hapo chini kwa kijarida hiki, tunatumia pia jukwaa la mawasiliano linaloitwa *Wacha Tuzungumze!* Kifaa hiki kiko na sifa inayowezesha watumiaji kuwasiliana na PPSD kwa usiri, ambacho kinaweza kusaidia yeyote anayeripoti habari muhimu au suala la usalama.

Mapema mwaka huu, Shule za Umma za Providence zilitoa ombi la pendekezo (RFP) ili mshauri wa usalama kutathmini mifumo yetu wilayani kote. Mtoa huduma atakayechaguliwa atafanya matembezi kwa kila jengo la PPSD wakati huu wa majira ya joto kufanya utathmini wa usalama. Tutafanya kazi na mtoa huduma kutengeneza mpango kuboresha usalama Wilayani kote.

Natamani tungeishi katika dunia ambapo itifaki hizi za usalama zisingekuwa za lazima shuleni. Lakini tafadhali fahamu ya kwamba timu yetu imejitolea kufanya kazi pamoja kuweka wanafunzi wetu na jamii yetu salama.

## TAARIFA MPYA ZA WILAYA

### KALENDA YA MASOMO YA MWAKA UJAO

Kalenda ya masomo ya mwaka 2022-23 iko hapa! Mwaka wa shule utaanza Jumatatu, Agosti 29, na utaishia Jumanne, Juni 21. Bofya kiungo hapa chini kupata maelezo kamili kuhusu tarehe za likizo za Wilaya, sikukuu, na kuruhusiwa mapema kwa masaa-2 kwa maendeleo ya taaluma ya wafanyakazi.

www.providenceschools.org/academiccalendar

### FURSA ZA KAZI KWA MAFUNZO YA MAJIRA YA JOTO

Tunafurahia kutoa mipango ya mafunzo ya majira ya joto kwa zaidi ya wanafunzi 3, 000 mwaka huu, na tunataka kusaidia kuziba pengo hili! Kuna nafasi kadhaa za kazi tunataka kukujulisha, hususan katika viwango vya darasa za msingi. Tafadhali fuatilia viungo hapa chini kutazama matangazo ya kazi za majira ya joto:

Wahitaji wa ndani bofya hapa

Wahitaji wa nje bofya hapa

### UNGANA NA PPSD KATIKA SIMU YAKO

Ungana na PPSD katika lugha yako kwa kutumia programu ya *Tuongee!* . Wanafunzi, familia, na wanajamii wanaweza pata majibu kupitia Kiarabu, Kichina (kilichorahisishwa), Kiingereza, Kifaransa. Kikhmer, Kirusi, Kihispania na Kivietnamu.


Kuna uwezekano pia kuwasilisha mazungumzo na kupokea majibu bila ya kujitambulisha kwa kuwasilisha ujumbe kama "Mteja Aliyefichwa." Maswali yote yanaelekezwa kwa mtaalam wa mada fulani, na msimamizi wa huduma ya wateja anachunguza kila uwasilishaji kuhakikisha majibu ya haraka. Programu ya*Tuongee!* inaweza kupakuliwa katika Apple au vifaa vya Android.

### 2022 KUHITIMU KWA SHULE ZA SEKONDARI KIDATO CHA SITA

Mwaka huu, sherehe zote za kuhitimu za PPSD zitafanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kisiwa cha Rhode. Kwa ratiba kamili ya kila sherehe ya shule, tafadhali tembelea www.providenceschools.org/graduations2022. Hongera kwa wanafunzi wetu wote wanaohitimu!

## KUWASHEREHEKEA WANAFUNZI

Wanafunzi wetu wenye bidii na wenye talanta wanafanya mambo ya ajabu kila siku! Hapa kuna mifano kadhaa.




### JROTC LINASHINDA TUKIO LA MASHINDANO


Kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2009, **Shirika la Mafunzo ya Maafisa Vijana wa Akiba** kadeti wa (JROTC) kwa Shule ya Upili/Sekondari ya Hope ilishinda **Tukio la Mashindano ya Raider** mkoani katika Shule ya Upili/Sekondari ya New Britain huko Connecticut! Mashindano ya Raider ni mashindano ya timu ambayo inaangazia uzoefu na ustahimilivu wa kimwili.

JROTC video: https://youtu.be/6fj6KDwrQp4



### MWEZI WA VITABU VYA RI LATINO

Kupitia ushirikiano na Rhode Island Center ya Sanaa za Latino, wanafunzi wa darasa la kwanza katika **Shule ya Msingi ya Lauro** walisherehekea **Mwezi wa Vitabu vya RI Latino** kwa kutembelewa na mteule wa mwaka 2022 wa Tuzo la Kitabu cha RI Latino, Emma Otheguy. Alisoma na kujibu maswali kuhusu kitabu chake kipya, *A Sled for Gabo/ Un trineo para Gabo* na kujadili kuhusu fasihi ya Latino.



### MASOMO YA URAIA

Wanafunzi kutoka masomo ya uraia katika **Jengo la Elimu la Juanita Sanchez (JSEC)** walihudhuria mkutano wa hivi majuzi wa Bodi ya Shule ya Providence kushawishi kuwa na usaidizi zaidi wa kiafya wa akili na programu za baada ya shule shuleni mwao. Wanafunzi walikuwa na majukumu kadhaa ikiwamo utafiti wa makala, ufikiaji kwa washirika wa jamii, ufikiaji wa kisheria na utafiti wa kijamii. Kupitia taarifa kutoka utafiti huu waliweza kupeana data safi na iliyo sahihi kusaidia maombi yao. Kazi nzuri sana!



## KUANGAZIA WAFANYAKAZI

Pata kujua watu wa ajabu wanaofanya kazi na wanafunzi wetu kila siku!

**Lindsay Paiva**

Mwalimu wa MLL wa darasa la Tatu

Aliye katika: Shule ya Msingi ya Mtaa wa Webster

Alijiunga na PPSD mnamo: 2017

***Kwanini unafanya kile unachofanya?***
Mimi ni mwalimu kwa sababu kwa maoni yangu, kuwaza kwa makini ni ujuzi muhimu sana ambao tunahitaji kama washirika wa jamii, na hususan kama vijana. Nasaidia watoto kwa kuwezesha kujifunza jinsi ya kuwaza kwa umakini, jinsi ya kuchambua mambo yanayowakumba. Natazama jukumu langu la kuinua wanafunzi wanaofahamu lugha nyingi (MLL) kama mfano wa jinsi tunavyopaswa kutamani kuwa. Wako na mitazamo tofauti na njia za kuchakata taarifa, kwa hivyo wanaweza kutia mkazo na kutafuta kuelewa wengine kwa sababu ya kufahamu lugha nyingi, na mtazamo wao kupitia tamaduni tofauti ambavyo wanaona dunia. Sikulelewa kama mwanafunzi anayefahamu lugha nyingi, lakini nadhani wakati nilipokuwa mtu mzima anayefahamu lugha nyingi na mwalimu wa MLL ilibadilisha uwezo wangu na kuniwezesha kuelewa dunia.

"Ni muhimu sana kwangu ya kwamba watoto wanapotoka darasa langu wanafahamu ya kwamba kuwa MLL ni rasilimali na jambo wanalopaswa kujivunia."

***Je, ni kwa nini kuwa mwalimu wa wanafunzi wanaofahamu lugha nyingi ni muhimu hivyo?***
Nadhani unapokuwa kijana mdogo anayefahamu lugha nyingi, shule inaweza kuchanganya. Ni muhimu sana kwangu ya kwamba watoto wanapotoka darasa langu wafahamu ya kwamba kuwa mjuzi wa lugha nyingi MLL ni rasilimali na jambo wanalopaswa kujivunia. Naweka msisitizo mkubwa kwa kukuza ufahamu wa lugha nyingi kwa sababu inafungua fursa na inajenga huruma na kuelewa mambo watu wanapitia. Mawasiliano ni ujuzi muhimu wa maisha na ni jinsi tunavyo tafuta kuelewana, kwa hivyo kuanza mapema na kusaidia wanafunzi kuweza kuwasiliana vyema inawapatia vifaa wanavyohitaji kufanikiwa maisha ya baadaye.

***Ni sehemu gani bora ya kazi yako?***
Watoto wanachekesha na hii inafurahisha sana katika ulimwengu huu uliojaliwa na uzito. Wanafurahisha sana na wanaleta furaha mno kwa sehemu tunayotumia pamoja. Wakati ninaopenda sana ni wakati tunaposoma na ninawaambia ni wakati wa kufanya jambo jingine, lakini wamependezwa sana na wanasema, "Je, hatuwezi kuongezwa dakika kumi zaidi?" Au wakati wanasherehekea wanafunzi wenzao – wao kwa wao ni washangiliaji wakuu. Wakati mmoja anaongeza kiwango cha kusoma au anachukua changamoto chanya, hao ndio wa kwanza kusifu na kusaidiana. Hii ndio sehemu ya kazi yangu inayovutia zaidi.

***Je, ungependa watu wengi kujua nini kuhusu kuwa mwalimu wa ESL?***
Kazi nyingi ya kufundisha huwa haionekani. Kwa watu walio nje ya elimu ningesema ya kwamba kufundisha ni zaidi ya masaa 6 kila siku na wanafunzi. Kufundisha ni uhusiano - unaweza kuwa na wanafunzi 26, lakini hao wanafunzi wameungana na watu wengi sana wengine ambao wana mchango mkubwa kwa maisha yao. Kwa hivyo kama mwalimu unapaswa kujitolea kufahamu kwa undani watoto hao, familia zao na ndugu zao na jamii pia. Ni jukumu letu kuelewa muktadha wa watoto walio mbele yetu, na kusaidia na kukuza maisha yao yote na tofauti zao zote.

## NI HABARI NJEMA: PPSD KWENYE VYOMBO VYA HABARI

- "Kuziba pengo": Wanafunzi wa kiufundi wanaleta upenzi wa uhandisi kwa wanafunzi wa shule ya kati
  Jarida la Providence, Mei 14, 2022
- 'Tayari kwa dunia ya kitaaluma': Shule ya Providence inawezesha mafunzo ya ujuzi
  Biashara ya Providence Kwanza, Mei 11, 2022
- Mkufunzi wa PC, Ed Cooley amepewa zawadi ya ufunguo wa jiji
  WPRI, Mei 17, 2022
- Redio ya Poder: DKT JAVIER MONTANEZ KWA EN EL CAN DE LA MAÑANA, ANAZUNGUMZA KUHUSU SHULE ZA PROVIDENCE
  Redio ya Poder, Mei 4, 2022

## WILAYANI



### MKUFUNZI COOLEY ANARUDI NYUMBANI

Asante sana kwa mkufunzi wa wanaume wa mpira wa vikapu wa **Chuo cha Providence** (na **mwanafunzi wa kale wa Shule ya Sekondari ya Central**) Ed Cooley kutembelea shule yake ya kale mwezi huu kuongea na wanafunzi wetu! Mkufunzi Cooley alipokea ufunguo wa heshima ya jiji la Providence kutoka kwa Meya Jorge Elorza. Halafu akaongea na wanafunzi kuhusu umuhimu wa kuweka malengo ya juu, kutokata tamaa, kushukuru kila siku, na kujivunia kuwa mwanafunzi wa PPSD.




### TUMAINI KUPITIA SANAA


Mtaalamu wa Jamii wa Shule ya Sekondari ya Hope Johnny Rivera na wasanii kadhaa wenyeji waliungana na wanafunzi kutengeneza sanaa kadhaa za kuchora ukutani kupamba kuta za ukumbi shuleni. Bofya kwenye picha hapo juu kutazama video ya mradi huu wa maajabu na mchango iliyo nayo kwa wanafunzi na jamii ya shule!
https://youtu.be/RQCIHy90Puo



### UBADILISHAJI WA LUGHA WA MZAZI/MWALIMU

Walimu na wazazi katika **Shule ya Msingi ya Lauro** wameunda timu kufanya mazoezi ya lugha lengwa (Kiingereza au Kihispania) kupitia vikao vya mazoezi vya vikundi vidogo. Vikundi hivi vinakutana mara mbili kila wiki baada ya shule. Hii inasaidia wazazi na walimu kujifunza lugha lengwa kama timu, hali ambayo inaboresha ufahamu wa tamaduni tofauti na inajenga uhusiano!


## SAMBAZA UJUMBE




### SHEREHE YA UENDESHAJI BAISKELI & UVAAJI HELMETI

**Jumapili, 5/29, kuanzia saa nne asubuhi (10 a.m.) hadi saa nane mchana ( 2 p.m.)**
**Dexter Field**
**71 Dexter Street, Providence**


Saidia watoto wetu kuwa salama msimu huu wa joto kwa kuhudhuria Sherehe ya Uendeshaji Baiskeli na Uvaaji Helmeti. Tukio linaonyesha michezo, muziki, lori za chakula, na **helmeti za bure za baiskeli**. Unaweza pia kujifunza kuhusu miradi ya jiji inayokuja, jinsi ya kubaki salama, na jinsi ya kusaidia jamii ya baiskeli. Jifunze zaidi >




### MAONYESHO YA KAZI YA PPSD

**Alhamisi, Juni 9, kutoka saa kumi na moja jioni (5 p.m) hadi saa moja jioni (7 p.m.)**
**DelSesto Middle School**
**152 Springfield Street, Providence**

Kuja ufanye uhusiano na viongozi wa shule na Timu ya Talanta ya Providence! Jifunze kuhusu fursa za kufundisha kwa mwaka wa Shule wa 2022-23, mchakato wa uwasilishaji wa maombi na uajiri, bonasi za waajiriwa wapya, na zaidi. Jisajili hapa >



### MAPUNGUZO YA BEI KWA WANAFUNZI NA WAFANYAKAZI

Wafanyakazi wa PPSD, wanafunzi na familia - ulijua ya kwamba umestahiki kwa mapunguzo kwa bidhaa fulani za Dell kupitia Mpango wa Ununuzi wa Elimu ya Dell?

Jifunze zaidi katika www.dell.com/PPSD-RI

## WEKA ALAMA KWENYE KALENDA ZAKO!

- **SIKU YA UKUMBUSHO - HAKUNA SHULE**
  Jumatatu, tarehe 30 Mei, 2022
- **MKUTANO WA BARAZA LA USHAURI LA WAZAZI (PAC)**
  Jumanne, Juni 21, 2022, saa kumi na mbili jioni (6:00 p.m.)
- **SIKU YA MWISHO YA WANAFUNZI**
  Jumatatu, Juni 13, 2022
- **MKUTANO WA BODI YA SHULE**
  Jumatano, Juni 22, 2022, saa kumi na mbili jioni (6:00 p.m.)
- **KUHITIMU KWA SHULE ZA UPILI/ SEKONDARI**
  Jumatatu, Juni 13 - Ijumaa, Juni 17
- **SIKU YA MWISHO YA MADARASA**
  Ijumaa, Juni 24, 2022

Mambo ya kusisimua yanatokea katika Wilaya nzima, na tunataka kueneza ujumbe! Ikiwa una programu, tukio, mfanyakazi, au mwanafunzi mwenye hadithi ya kushangaza ambayo ungependa kuangazia, tafadhali tuma barua pepe kwa communications@ppsd.org.

Providence Schools

© 2022 Providence Public Schools · communications@ppsd.org · www.providenceschools.org